

THINK OF SOCIAL COHESION

Washirika waandaaji



Summit Architect



Mshirika wa vyombo vya habari



RASIMU YA MASHAURIANO

Mpango Elekezi Unaoibuka wa Mshikamano wa Kijamii

Tarehe 16 Oktoba hadi 6 Novemba 2026

RASIMU YA TAFSIRI. Bado haijathibitishwa na NAATI. Kwa ajili ya kukaguliwa na washirika waandaaji kabla ya kuchapishwa. Maandishi ya Kiingereza ndiyo toleo rasmi.

DRAFT TRANSLATION. Not yet NAATI certified. For checking by the convening partners before publication. The English text is the authoritative version.

→ Yaliyomo

Mpango Elekezi	3
Vipaumbele vitano, hatua tano zinazopendekezwa	4
Mahali Mpango Elekezi huu unapoanzia	5
1 Haki na wajibu	6
2 Kuwafikia watu	7
3 Ushiriki	8

4 Uwajibikaji	9
5 Simulizi	10
Mapendekezo mawili ya kushikilia pamoja	11
Kupanua mashauriano haya	11
Tunachowauliza	12

Imetolewa kwa ajili ya mashauriano na SydWest, SSI na SCOA. Rasimu hii ya mashauriano inaendeleza vipaumbele vitano vinavyoibuka vilivyobainishwa kupitia Mkutano wa Kilele (Summit) na Ripoti ya Mkutano wa Kilele, na inapendekeza hatua moja chini ya kila kimoja. Vipaumbele hivyo wala hatua hizo hazijawasilishwa kama zilizoidhinishwa au kuthibitishwa kikamilifu na Mkutano wa Kilele. Sasa zinarudishwa kwa ajili ya kutafakariwa na kurekebishwa zaidi. Kwa makusudi, rasimu hii si ya mwisho: kila kipengele cha mfumo huu kiko wazi kwa marekebisho kupitia mashauriano haya.

Mkutano wa Kilele wa Kitaifa wa Think Social Cohesion (Fikiria Mshikamano wa Kijamii) ulionyesha kuwa Australia haikosi mawazo. Inakosa mfumo wa kuchukua hatua ambao ni wa pamoja vya kutosha na wenye uwajibikaji.

Tarehe 28 Julai 2026, viongozi 160 walioalikwa walitumia siku nzima Parramatta wakichunguza hali zinazoimarisha au kudhoofisha mshikamano wa kijamii. Ingawa majadiliano hayakufikia makubaliano kuhusu kila suala, vipaumbele vitano vilivyo wazi viliibuka mara kwa mara katika hotuba kuu, majadiliano ya jopo na michango ya washiriki. Vipaumbele hivi vinatoa msingi wa pamoja wa kuchukua hatua, huku vikitambua kuwa tofauti muhimu za mitazamo bado zipo na zinahitaji kutafakariwa zaidi. Vipaumbele hivyo vitano vimewekwa hapa chini kama mfumo unaoibuka, kila kimoja kikifuatiwa na hatua moja inayopendekezwa na maswali ambayo sasa tunawaomba myajaribu.

Kila hatua inayopendekezwa ina maelezo kuhusu chimbuko lake: matokeo ya mkutano wa kilele, pendekezo ambalo washirika waandaaji wameliendeleza tangu wakati huo, au yote mawili. Ripoti ya Mkutano wa Kilele ndiyo kumbukumbu ya siku hiyo; Mpango Elekezi huu unaeleza jinsi tunavyopendekeza kuendeleza hatua hizo. Kila hatua itaendelezwa kama nyanja yake ya kazi, na mashirika yataalikwa kuchangia.

Vipaumbele vitano, hatua tano zinazopendekezwa

Kujenga mazingira ya kuwa sehemu ya jamii, ushiriki na uaminifu

Mkutano wa Kilele wa Kitaifa wa Think Social Cohesion (Fikiria Mshikamano wa Kijamii) ulionyesha kuwa Australia haikosi mawazo. Inakosa mfumo wa kuchukua hatua ambao ni wa pamoja vya kutosha na wenye uwajibikaji. Kwa makusudi, rasimu hii si ya mwisho: kila kipengele cha mfumo huu kiko wazi kwa marekebisho kupitia mashauriano haya.

Kipaumbele 1

Haki na wajibu

Mfumo lazima uhakikishe nini?

Kutoka mkutano wa kilele

Katika majadiliano yote, washiriki walisisitiza mara kwa mara umuhimu wa haki, wajibu na uwajibikaji wa kitaasisi.

Hatua inayopendekezwa

Kuanzisha mfumo wa haki na wajibu wa kitaasisi kwa ajili ya mshikamano wa kijamii

Kipaumbele 2

Kuwafikia watu

Ni nani ambao tunashindwa kuwafikia?

Kutoka mkutano wa kilele

Swali gumu zaidi, lililojitokeza lenyewe katika vikao vinne tofauti, ni jinsi ya kuwafikia wale ambao taasisi na programu zilizopo bado hazijawafikia.

Hatua inayopendekezwa

Kuwekeza katika miundombinu ya mtaa inayowafikia watu

Kipaumbele 3

Ushiriki

Watu huchangia vipi?

Kutoka mkutano wa kilele

Utambuzi wa ujuzi na sifa za kitaaluma kutoka nje ya nchi ulikuwa pendekezo lenye ushahidi imara zaidi la mkutano wa kilele, lililobuliwa katika vikao vitano bila pingamizi lolote lililorekodiwa.

Hatua inayopendekezwa

Kuwezesha matumizi ya ujuzi na kuondoa vikwazo vya ushiriki

Kipaumbele 4

Uwajibikaji

Ni nani anayewajibika kwa matokeo?

Kutoka mkutano wa kilele

Kama mshiriki mmoja alivyosema, kusikiliza hakukamiliki hadi watu waone kilichobadilika kwa sababu walizungumza.

Hatua inayopendekezwa

Kutumia utaratibu wa uwajibikaji kwa kila ahadi ya Mpango Elekezi

Kipaumbele 5

Simulizi

Ni hadithi gani inayowezesha haya yote?

Kutoka mkutano wa kilele

Mkutano wa kilele ulikwenda zaidi ya wito wa hadithi bora. Ulibainisha sifa za kimuundo za mazingira ya habari, ikiwa ni pamoja na algoriti zilizoundwa kuchochea hasira, motisha za kibiashara na muundo wa majukwaa unaoweza kuzigombanisha jamii, na ulibua wajibu wa kujali katika mazingira ya kidijitali kama mwitikio mmoja wa kimuundo unaowezekana.

Hatua inayopendekezwa

Kuendeleza na kukuza mfumo wa kusimulia hadithi kwa maadili, na mwitikio wa kimuundo kwa mazingira ya habari

Mahali Mpango Elekezi huu unapoanzia

Mfumo wowote wa Australia wa mshikamano wa kijamii lazima uanze kwa kutambua Waaborijini (Aboriginal) na Wakazi wa Visiwa vya Mlango-bahari wa Torres (Torres Strait Islander) kama Watu wa Kwanza wa bara hili, na kwa maelezo ya kweli ya ukoloni, unyang'anyi wa ardhi na mamlaka kuu inayoendelea. Pendekezo hili limewekwa hapa ili lijaribiwe.

Kila ahadi hubeba

kiongozi mmoja aliyetajwa anayewajibika

mshirika mmoja mwenye uzoefu wa moja kwa moja wa suala husika

rasilimali zinazohitajika

kiwango cha kuanzia

kipimo cha miezi sita

njia ya uwazi ya kuripoti maendeleo

→ Mahali Mpango Elekezi huu unapoanzia

Tangu mkutano wa kilele, washirika waandaaji wamependekeza kuwa mamlaka kuu ya Mataifa ya Kwanza (First Nations) na usemaji wa ukweli vinapaswa kuwa ndani ya msingi wa kidhana wa Mpango Elekezi huu, badala ya kuwa miongoni mwa sauti zitakazoongezwa kupitia mashauriano. Mkutano wa kilele wenyewe ulirekodi kuwa maarifa na uongozi wa Mataifa ya Kwanza vilihitaji umakini mkubwa zaidi kuliko vilivyopata siku hiyo. Pendekezo hili limewekwa hapa ili lijaribiwe.

Pendekezo hili litaendelezwa zaidi kupitia ushirikishwaji wa heshima na viongozi na mashirika ya Mataifa ya Kwanza kabla Mpango Elekezi haujakamilishwa. Kuanzisha ubia wenye maana wa utawala kunahitaji muda, uaminifu na ushirikiano wa kweli, na hakuwezi kufikiwa kupitia mchakato mfupi wa mashauriano. Mpango Elekezi utabainisha uendelezaji wa ubia huu kama kipaumbele cha awali cha utekelezaji.

Chanzo: pendekezo lililoendelezwa na washirika waandaaji tangu mkutano wa kilele.

Pendekezo la kujaribiwa

Mfumo wowote wa Australia wa mshikamano wa kijamii lazima uanze kwa kutambua Waaborijini (Aboriginal) na Wakazi wa Visiwa vya Mlango-bahari wa Torres (Torres Strait Islander) kama Watu wa Kwanza wa bara hili, na kwa maelezo ya kweli ya ukoloni, unyang'anyi wa ardhi na mamlaka kuu inayoendelea. Hisia ya kuwa sehemu ya jamii haiwezi kujengwa juu ya kusahau historia. Usemaji wa ukweli, kujiamulia na mahusiano ya heshima kati ya watu wa Mataifa ya Kwanza na wale wote ambao baadaye wamejenga maisha yao hapa ni msingi wa mustakabali wa pamoja wa taifa.

Kipaumbele 1

→ Haki na wajibu

Mfumo lazima uhakikishe nini?

Mshikamano wa kijamii hauwezi kutegemea nia njema, matarajio au kauli za jumla za maadili pekee. Katika majadiliano yote, washiriki walisitiza mara kwa mara umuhimu wa haki, wajibu na uwajibikaji wa kitaasisi. Hii ilijumuisha wito wa ulinzi imara zaidi wa kisheria na unaozingatia haki, na wa waajiri kuwa na wajibu chanya wa kuzuia ubaguzi wa rangi, badala ya kuchukua hatua tu baada ya madhara kutokea. Pendekezo linaloibuka ni kwamba mbeba wajibu anapaswa kutajwa kwa kila ahadi, badala ya wajibu kuwaelekea watu wanaopata madhara.

Mkutano wa kilele haukupendekeza kuwa sheria pekee huunda mshikamano. Mchango mmoja ulipinga waziwazi mwitikio unaotegemea zaidi sheria. Mwelekeo si sheria badala ya mahusiano, bali msingi imara zaidi wa haki ukiambatana na hali za kijamii na za kitaasisi zinazowezesha haki hizo kupatikana kivitendo.

Hatua inayopendekezwa · kwa kujaribiwa

Kuanzisha mfumo wa haki na wajibu wa kitaasisi kwa ajili ya mshikamano wa kijamii

Kumtaja mbeba wajibu kwa kila wajibu, na kuchunguza hoja ya wajibu chanya wa kuzuia ubaguzi wa rangi kwa waajiri na taasisi nyingine. Muundo wa chombo chochote kipana zaidi cha haki bado uko wazi. Mwitikio wowote wa kisheria unapaswa kuendelezwa sambamba na mbinu zinazozingatia mahusiano na maeneo ambazo mkutano wa kilele ulibainisha, si kama mbadala wake.

Chanzo: matokeo ya mkutano wa kilele (Ripoti ya Mkutano wa Kilele, sehemu 3.1 na 6.1). Mkutano wa kilele ulitaka aina fulani ya chombo cha kisheria au kinachozingatia haki na haukuamua muundo wake.

Kwa mashauriano

- Je, hii inaakisi majadiliano? Chombo cha haki kinapaswa kuchukua muundo gani, na wajibu chanya unapaswa kutumika wapi?

Kipaumbele 2

→ Kuwafikia watu

Ni nani ambao tunashindwa kuwafikia?

Mipango ya mshikamano wa kijamii mara nyingi huwafikia watu ambao tayari wana nia na uwezo wa kushiriki. Swali gumu zaidi, lililojitokeza lenyewe katika vikao vinne tofauti, ni jinsi ya kuwafikia wale ambao taasisi na programu zilizopo bado hazijawafikia: watu ambao wamejitenga, wale ambao mbinu zilizopo hazijawafaa, na wale ambao hawajawahi kufikiwa kwa namna yenye maana.

Mkutano wa kilele ulisisitiza umuhimu wa kutofautisha uzoefu huu, ukitambua kuwa unaakisi vikwazo tofauti vya ushiriki na unahitaji majibu tofauti. Muhimu zaidi, ukosefu wa ushiriki haupaswi kudhaniwa kuwa ukosefu wa nia ya kushiriki.

Watu hufikiwa kupitia mahali, huduma na mashirika yaliyo karibu nao, katika maeneo wanamoishi. Serikali za mitaa, mashirika ya mtaa, maktaba, shule, mahali pa kazi, vyombo vya habari vya mtaa, maeneo ya kukutania nje ya nyumbani na kazini, na mipango ya ngazi ya mtaa kama vile ruzuku ndogo ndogo, ndipo watu hukutana na taasisi na wao kwa wao. Kwa watu wanaojenga maisha yao hapa, miundombinu ya huduma za kuwasaidia watu wanaoanza maisha mapya Australia ndiyo daraja kuelekea jamii, huduma na taasisi. Ili kuwafikia watu hawa, taasisi zinapaswa kubadilisha mahali, jinsi na kupitia nani zinavyowashirikisha watu.

Hatua inayopendekezwa · kwa kujaribiwa

Kuwekeza katika miundombinu ya mtaa inayowafikia watu

Kuimarisha serikali za mitaa, mashirika ya mtaa, maktaba, shule, mahali pa kazi na maeneo ya kukutania nje ya nyumbani na kazini, huku taasisi zikitakiwa kuchunguza na kuimarisha mahali, jinsi na kupitia nani zinavyowashirikisha watu, kwa umakini maalum kwa watu ambao hawajafikiwa kupitia mitandao iliyopo.

Chanzo: matokeo ya mkutano wa kilele (Ripoti ya Mkutano wa Kilele, sehemu 3.2 na 6.2).

Kwa mashauriano

- Ni nani wanaoachwa nje katika jamii au sekta yako, na ni nini kingewafikia?
- Ni miundombinu gani ya mtaa ambayo Mpango Elekezi unapaswa kuipa kipaumbele katika uwekezaji?

Kipaumbele 3

→ Ushiriki

Watu huchangia vipi?

Utambuzi wa ujuzi na sifa za kitaaluma kutoka nje ya nchi ulikuwa pendekezo lenye ushahidi imara zaidi la mkutano wa kilele, lililoibuliwa katika vikao vitano bila pingamizi lolote lililorekodiwa. Uwezo usipoweza kugeuzwa kuwa fursa, matokeo yake huathiri usalama wa kiuchumi, kujitegemea, kujiamini na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maisha ya Australia. Mkutano wa kilele ulielekeza kwenye njia za kusonga mbele badala ya huduma: mifumo iliyobuniwa kwa kuzingatia maendeleo ya watu, uwezo wao wa kujiamulia na uwezo wao wa kuchangia, ikiwa ni pamoja na kupitia ajira na ujasiriamali.

Ushiriki ni mpana zaidi kuliko ushiriki wa kiuchumi. Unajumuisha uongozi wa kijamii na wa kiraia na fursa za kweli za kuchagiza taasisi na maamuzi yanayoathiri maisha ya watu. Mkutano wa kilele pia ulikiri pengo muhimu katika majadiliano: hali za kimaisha zinazounda mshikamano wa kijamii, ikiwa ni pamoja na makazi, mishahara, kazi zisizo na uhakika na shinikizo la gharama za maisha, zilipata umakini mdogo kulinganisha na masuala mengine. Masuala haya yatahitaji kutafakariwa kwa makusudi zaidi kadri Mpango Elekezi unavyoendelezwa.

Hatua inayopendekezwa · kwa kujaribiwa

Kuwezesha matumizi ya ujuzi na kuondoa vikwazo vya ushiriki

Kuanza na utambuzi wa ujuzi na sifa za kitaaluma kutoka nje ya nchi, kujenga njia za kuingia katika uongozi wa kiraia na wa kijamii pamoja na ajira, na kuchunguza hali za kimaisha zinazozuia ushiriki.

Chanzo: matokeo ya mkutano wa kilele (Ripoti ya Mkutano wa Kilele, sehemu 3.3 na 6.3).

Kwa mashauriano

- Ni nini kingegeuza uwezo uliopo kuwa ushiriki kwa haraka zaidi?
- Hali za kimaisha na za kiuchumi zinapaswa kuingizwa vipi katika mfumo huu?

Kipaumbele 4

→ Uwajibikaji

Ni nani anayewajibika kwa matokeo?

Katika vikao vitano, washiriki walieleza wasiwasi kuwa mashauriano mara nyingi hushindwa kugeuka kuwa hatua zenye maana. Watu huchangia muda wao, uzoefu na utaalamu, lakini mara chache huona jinsi michango yao inavyoathiri maamuzi au kuleta mabadiliko. Mkutano wa kilele ulisisitiza haja ya kwenda zaidi ya mashauriano yenye maana hadi uwajibikaji wa kweli: ni nani anayechukua jukumu la kutenda kulingana na yaliyosikika, na wale waliochangia wanawezaje kuona matokeo? Kama mshiriki mmoja alivyosema, kusikiliza hakukamiliki hadi watu waone kilichobadilika kwa sababu walizungumza.

Kikao cha kufunga kiliipa kanuni hii umbo lake halisi zaidi. Washiriki walipendekeza kuwa kila ahadi ya Mpango Elekezi inapaswa kuwa na utaratibu wa uwajibikaji:

- kiongozi mmoja aliyetajwa anayewajibika
- mshirika mmoja mwenye uzoefu wa moja kwa moja wa suala husika
- rasilimali zinazohitajika
- kiwango cha kuanzia
- kipimo cha miezi sita
- njia ya uwazi ya kuripoti maendeleo.

Pendekezo ni kwamba utaratibu huu utumike kwa kila ahadi iliyotolewa katika Mpango Elekezi wa mwisho. Ahadi isiyo na mtu au taasisi iliyotajwa kuwajibika kwa utekelezaji wake, rasilimali zinazohitajika na njia ya kupima maendeleo ni nia tu, si mpango elekezi.

Mpango Elekezi Unaoibuka wa Mshikamano wa Kijamii • Rasimu ya mashauriano

Hatua inayopendekezwa • kwa kujaribiwa

Kutumia utaratibu wa uwajibikaji kwa kila ahadi ya Mpango Elekezi

Kila ahadi hubeba kiongozi aliyetajwa anayewajibika, mshirika mwenye uzoefu wa moja kwa moja wa suala husika, rasilimali zinazohitajika, kiwango cha kuanzia, kipimo cha maendeleo na njia ya uwazi ya kuripoti, na washiriki wanaelezwa kilichobadilika kwa sababu walichangia.

Chanzo: matokeo ya mkutano wa kilele kutoka kikao cha kufunga (Ripoti ya Mkutano wa Kilele, sehemu 3.4 na 6.4). Wajibu chanya wa kuzuia ubaguzi wa rangi uko chini ya Haki na wajibu, mahali ambapo mkutano wa kilele uliweka.

Kwa mashauriano

- Je, huu ndio utaratibu sahihi wa uwajibikaji, na ni nini kingeufanya uwe wa lazima na wenye uwajibikaji unaoweza kudaiwa, badala ya kubaki matarajio tu?

Kipaumbele 5

→ Simulizi

Ni hadithi gani inayowezesha haya yote?

Australia inahitaji hadithi ya kitaifa yenye uwezo wa kubeba usemaji wa ukweli, tamaduni mbalimbali, hisia ya pamoja ya kuwa sehemu ya jamii, na kutofautiana kwa maoni kunakokubalika. Jinsi tunavyozungumzia utofauti huunda uelewa wa umma, sera na hisia ya kuwa sehemu ya jamii, na uongozi wa kisiasa na wa kitaasisi husaidia kuweka mipaka ya kile ambacho mazungumzo ya umma huhalalisha.

Mkutano wa kilele ulikwenda zaidi ya wito wa hadithi bora. Ulibainisha sifa za kimuundo za mazingira ya habari, ikiwa ni pamoja na algoriti zilizoundwa kuchochea hasira, motisha za kibiashara na muundo wa majukwaa unaoweza kuzigombanisha jamii, na uliibua wajibu wa kujali katika mazingira ya kidijitali kama mwitikio mmoja wa kimuundo unaowezekana. Pia ulitoa pendekezo moja linaloweza kutekelezwa mara moja: itifaki ya kusimulia hadithi kwa maadili iliyojengwa juu ya ridhaa inayotolewa kwa ufahamu na inayoendelea, usalama wa kitamaduni, uandishi wa pamoja, utambuzi unaostahili na haki ya kupitia upya au kujiondoa, ambayo mashirika yanaweza kuanza kuitumia bila kusubiri sheria au ufadhili.

Hatua inayopendekezwa · kwa kujaribiwa

Kuendeleza na kukuza mfumo wa kusimulia hadithi kwa maadili, na mwitikio wa kimuundo kwa mazingira ya habari

Kujenga mfumo huo juu ya ridhaa inayotolewa kwa ufahamu na inayoendelea, usalama wa kitamaduni, uandishi wa pamoja, utambuzi unaostahili na haki ya kupitia upya au kujiondoa. Sambamba nao, kuendeleza mwitikio wa kimuundo unaohusu motisha za majukwaa, jinsi algoriti zinavyokuza maudhui na wajibu wa vyombo vya habari, pamoja na simulizi ya umma iliyojaribiwa ya kuwa sehemu ya jamii na kuchangia.

Chanzo: matokeo ya mkutano wa kilele (Ripoti ya Mkutano wa Kilele, sehemu 3.5 na 6.5).

Kwa mashauriano

- Je, Mpango Elekezi unapaswa kutafuta miitikio ya kimuundo kwa mazingira ya habari, na ipi?
- Je, shirika lako lingeunga mkono au kupitisha itifaki ya kusimulia hadithi kwa maadili inayozingatia kanuni hizi?
- Mpango Elekezi unapaswa vipi kulinda usalama na heshima huku ukihifadhi nafasi ya kutofautiana kwa maoni kunakokubalika na mazungumzo magumu?

→ Mapendekezo mawili ya kushikilia pamoja

Katika Mkutano wote wa Kilele, kanuni mbili muhimu na zinazohusiana kwa karibu ziliibuka, zikionyesha mvutano unaopaswa kushughulikiwa kwa uangalifu. Mshikamano wa kijamii ni wa Waaustralia wote: ni wajibu wa jamii nzima na haupaswi kuelezwa kama kitu ambacho jamii za wahamiaji na za tamaduni mbalimbali ndizo zinazowajibika kukijenga. Wakati huo huo, uwepo wa tamaduni mbalimbali ni nguvu ya kitaifa inayoitambulisha Australia, ambayo inapaswa kuingizwa kwa kina zaidi ndani ya mifumo, taasisi na maisha ya umma ya Australia. Kazi iliyo mbele ni kushikilia yote mawili: kutambua na kuimarisha tabia ya Australia ya tamaduni mbalimbali huku ikiwekwa wazi kuwa wajibu wa mshikamano hauwezi kubebeshwa jamii za tamaduni mbalimbali pekee.

→ Kupanua mashauriano haya

Mkutano wa Kilele ulitoa msingi muhimu wa majadiliano, huku ukitambua kuwa siku moja haikuweza kunasa wigo kamili wa mitazamo na uzoefu unaounda mshikamano wa kijamii Australia. Maeneo kadhaa yalipata umakini mdogo au hayakuwakilishwa vya kutosha, ikiwa ni pamoja na maarifa na uongozi wa Mataifa ya Kwanza, watu wenye ulemavu, vijana, jamii za mikoani na vijijini, jamii ndogo za kidini, hali za kimaisha na za kiuchumi, na mbinu za ushahidi na vipimo.

Mchakato wa mashauriano unalenga kushughulikia mapengo haya kupitia michango ya maandishi iliyolengwa na ushirikishwaji wa watu na mashirika ambayo mitazamo yao haikuwakilishwa vya kutosha, ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji maalum wa viongozi na mashirika ya Mataifa ya Kwanza. Tunahimiza hasa michango kutoka kwa makundi haya ili kuhakikisha Mpango Elekezi wa mwisho unaakisi wigo mpana zaidi wa uzoefu, vipaumbele na utaalamu, na unaimarishwa na sauti ambazo hazikusikika vya kutosha siku hiyo.

→ Tunachowauliza

- Je, kila hatua inayopendekezwa inaakisi tatizo? Ni nini kinakosekana au kimetiliwa chumvi?
- Ni hatua zipi zilizo muhimu zaidi kwa watu ambao shirika lako linafanya nao kazi?
- Ni nini kinapaswa kubadilika kabla Mpango Elekezi haujakamilishwa?
- Hatua inayofuata inahitaji kusikia mitazamo ya nani?
- Hiari: je, shirika lako lingependa kuchangia katika mojawapo ya nyanja tano za kazi, na ipi?

Jinsi ya kushiriki

16 Oktoba 2026	Mashauriano yanafunguliwa kwa kikao cha moja kwa moja katika kongamano la FECCA. Mikondo mitano inawasilishwa kwa wahudhuriaji.
19 Oktoba 2026	Utafiti unatumwa kwa washiriki wa Mkutano wa Kilele na mitandao ya washirika waandaaji.
6 Novemba 2026	Mashauriano yanafungwa. Kila hoja ya msingi inarekodiwa na kupewa matokeo yaliyoandikwa.
Baada ya mashauriano	Ripoti ya 'tulichosikia, kilichobadilika' inatumwa kwa kila mjibu. Ramani ya mwisho inawasilishwa kwa Tume ya Kifalme ya Chuki dhidi ya Wayahudi na Mshikamano wa Kijamii na kwa serikali.
Miezi sita baadaye	Ahadi zinaripotiwa kwa kufuata muundo wa uwajibikaji.

Jinsi mashauriano haya yanavyoendeshwa

Mashauriano yanafunguliwa kwa kikao cha ana kwa ana katika kongamano la FECCA tarehe 16 Oktoba 2026, ambapo vipaumbele vitano na hatua zinazopendekezwa zinawasilishwa kwa wahudhuriaji kama nyanja tano za kazi na kujaribiwa kupitia majadiliano na dodoso la mashauriano. Majibu yanayotolewa ukumbini ni mawasilisho rasmi. Kisha dodoso linatumwa kwa washiriki wa Mkutano wa Kilele na mitandao ya washirika waandaaji tarehe 19 Oktoba 2026 na kufungwa tarehe 6 Novemba 2026. Majibu yanaweza kutolewa kupitia dodoso la mashauriano kwenye thinksocialcohesion.com.au, ambalo linauliza maswali yaliyo hapo juu. Kikundi kazi cha washirika waandaaji watatu na mbunifu wa dhana na mbinu za Mkutano wa Kilele (Summit Architect) kitapitia kila jibu. Kila hoja ya msingi itarekodiwa katika rejista ya maoni na kupewa matokeo yaliyoandikwa: imekubaliwa, imerekebishwa, au haijakubaliwa, pamoja na sababu.

Kila atakayetoa jibu na kuacha anwani ya barua pepe atapokea ripoti ya 'tulichosikia, kilichobadilika', inayoonyesha jinsi maoni ya mashauriano yalivyounda Mpango Elekezi wa mwisho, na Mpango Elekezi wa mwisho utawasilishwa kwa Tume ya Kifalme ya Chuki dhidi ya Wayahudi na Mshikamano wa Kijamii (Royal Commission on Antisemitism and Social Cohesion) na kwa serikali. Mkutano wa Kilele awali ulipendekeza mapitio ya uwajibikaji ya miezi sita, yaliyopangwa tarehe 28 Januari 2027. Hata hivyo, kwa kuwa Mpango Elekezi unakamilishwa baadaye kuliko ilivyotarajiwa, mapitio wakati huo yangetoa muda usiotosha kwa ahadi kutekelezwa na maendeleo kutathminiwa kwa namna yenye maana. Kwa hiyo mapitio yatafanyika miezi sita baada ya kuchapishwa kwa Mpango Elekezi wa mwisho, ambapo maendeleo ya ahadi yatathminiwa na kuripotiwa hadharani kupitia mfumo wa uwajibikaji wa Mpango Elekezi. Hii itatoa kipimo muhimu cha iwapo ahadi zilizotolewa zinageuka kuwa hatua zenye maana na matokeo yanayoonekana.